# AGANO LA USHIRIKA WA KANISA ANGALIKANA

## Utangulizi wa Agano

*"na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia , na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu); hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo. Na haya twayaandika, ili furaha yetu itimizwe"*.(1Yn.1:2-4).

1. Mungu ametuita tuingie katika Ushirika wa Mwanawe Yesu Kristo (1Kor.1:9). Ushirika huu "umedhihirishwa kwetu" na Mwanawe kuwa ni uzima wa milele wa Mungu wa Utatu. Ni uzima gani uliodhihirishwa kwetu? Mtakatifu Yohana anafafanua wazi kuwa Ushirika wa uzima wa milele katika Kanisa umo katika Ushirika wa Mungu mwenyewe katika Utatu Mtakatifu. Uzima huu hauko mbali nasi bali ni uzima ambao "umeonekana na kushuhudiwa" na Mitume na wafuasi wao; kwa kuwa katika Ushirika wa Kanisa tunashiriki katika Uzima wa milele."[1] Uzima huu wa Mungu mmoja, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu huongoza na hujidhihirisha katika kuwepo kwa Kanisa na huduma yake.

2. Wito wetu Mtakatifu katika Ushirika unathibitishwa katika makusudi ya Mungu kwa ulimwengu wote. (Ef. 1:10;3,9f). Unawafikia wanadamu wote ili, kushiriki kwetu uzima wa Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, kuweze kuturejeshea sura yetu ya Uungu. Maandiko Matakatifu yanaonyesha kuwa wakati wote Mungu ameendeleza wito huu kwa kutumia mapatano na Noha, Ibrahim, Israel na Daudi. Nabii Yeremia alitaraji kuliona Agano Jipya lisiloandikwa katika vibao vya mawe bali katika mioyo (Yer 31:31-34). Katika Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, tumepewa Agano Jipya, lililowekwa kwa damu yake *"imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi, lililoimarishwa kwa ufufuo wake kutoka kwa wafu"*. (Ef.1:19-23). *Na kutiwa muhuri, kwa kipawa cha roho Mtakatifu kilichomiminwa katika mioyoni yetu* (Rum 5:5). Katika Agano hili la kufa katika dhambi na la uzima mpya katika Kristo tunabatizwa, na tunawezeshwa kuingia katika Ushirika wa Mungu katika Kristo na watu wote, hata miisho yote ya dunia na ya uumbaji.

3. Kwa unyenyekevu tunatambua kuwa wito huu na kipawa cha Ushirika vinatupa wajibu wa aina mbalimbali kwa maisha yetu ya pamoja mbele za Mungu tunapohitaji, kwa njia ya neema, kuwa waaminifu katika huduma yetu ya kutekeleza makusudi ya Mungu kwa ulimwengu. Kwa kuunganishwa katika Kanisa moja la mahali pote, ambalo ni Mwili wa Kristo, lililoenea pande zote za dunia, tunaihudumia Injili ya Kristo, hata katika kuwezeshwa kuwa wamoja katikati ya kuta za dhambi ya binadamu zinazotugawanya na kututenganisha (Ef.2:12-22). Sura mbalimbali za maisha haya katika Kanisa linaloishi katika siri ya Ushirika Mtakatifu, zina ifunua "Hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa Roho unaopiga vita na kuligawanya kanisa". (Ef.3:9-10). Uaminifu, uadilifu, utu wema, unyenyekevu, uvumilivu, msamaha, na upendo wenyewe vinavyoonyeshwa katika maisha ya kuheshimiana na kuhudumiana kati ya watu wa Kanisa na kwa kupitia huduma zake mbalimbali; (Mark 10:44-45 ) vyote hivi huchangia kuujenga Mwili wa Kristo kadri unavyoendelea kukua na kufikia utimilifu (Ef.4:1-16; Kol.3:8-17).

4. Historia inaonyesha kuwa jamii mbalimbali za Makanisa zinaendelea kukua katika Kanisa lililoenea ulimwenguni kote. Miongoni mwa jamii hizi ni Ushirika wa Waanglikana unaodhihirisha nguvu maalum na mshikamano kati ya wafuasi na watumishi wengi wa Kristo. Tunatambua maajabu, uzuri na changamoto ya kudumisha ushirika huu wa jamii hii ya Makanisa na haja ya kila mmoja kujitoa na kujizatiti kuwa shahidi wa ahadi ya Mungu katika ulimwengu na nyakati zinazotetemeshwa, zenye migongano na mafarakano. Kwa hiyo tunafanya Agano kwa pamoja tukiwa Makanisa ya Ushirika wa Waanglikana kuwa waaminifu kwa ahadi za Mungu, kwa kushika Imani ya Mitume tunayoikiri, Ibada zetu za pamoja, Ushirikiano wetu katika Utume wa Mungu na namna tunavyoishi pamoja.

5. Kuweka Agano la pamoja hakukusudii kubadilisha sura ya Uanglikana inayoonyesha Imani ya Kikristo. Bali tunatambua umuhimu wa kuhuwisha kwa dhati Mshikamano wetu wa kila mmoja na mwenzake na uelewo wetu wa pamoja wa imani na huduma tuliyoipokea ili vifungo vya upendo vinavyo tushikamanisha pamoja viweze kuthibitishwa na kuimarishwa. Tunafanya hivyo ili kuonyesha uhusiano wetu wa kila mmoja na mwenzake, uaminifu na ahadi za Mungu mwenyewe kwetu sisi katika Kristo (2Kor 1:20-22).

6. Sisi ni watu tunaoishi, na kujifunza, na kusali, kwa kutumia Maandiko Matakatifu ambayo ni Neno la Mungu . Tunalenga kumtukuza Mungu kwa shukrani na kumsifu na kufanya maombezi kwa ajili ya mahitaji ya watu popote pale kwa njia ya sala ya pamoja, tukiunganishwa pamoja watu wa tamaduni na lugha mbalimbali. Tumepewa upendeleo wa kushiriki katika Utume wa Mitume kuipeleka Injili ya Kristo kwa Mataifa na watu wote, sio tu kwa maneno bali pia kwa matendo ya huruma na haki yanayoshuhudia tabia ya Mungu na ushindi wa Kristo dhidi ya dhambi na mauti. Tunajitoa kuwa wahudumu wa Umoja wa Kanisa miongoni mwa Wakristo waliogawanyika katika ulimwengu. Mungu na atusaidie "tusijihubiri wenyewe bali Kristo Yesu kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu" (2Kor 4:5).

7. Imani yetu ina ushuhuda thabiti wa yale tuliyopokea kutoka Neno la Mungu na ushuhuda wa muda mrefu wa Kanisa. Maisha yetu ya pamoja yanaonyesha baraka za Mungu katika kuukuza ushirika wetu hata kuwa kweli jamii ya ulimwengu wote (pamoja na kuonyesha mapungufu yetu katika imani, tumaini, na upendo). Utume tunaoufuata unalenga kuhudumia ahadi kuu za Mungu katika Kristo zinazowakumbatia watu wote na ulimwengu ambao Mungu anaupenda. Utume huu unatekelezwa katika uwajibikaji wa pamoja na uwakili wa vipawa vya Mungu na katika kutegemezana kati yetu na Kanisa lote ulimwenguni.

8. Sala yetu ni kwamba, Mungu atabariki jitihada zetu na kutukomboa katika udhaifu wetu, atahuisha na kutajirisha maisha yetu ya pamoja, na atatumia Ushirika Anglikana, ukifanya kazi na watu wote wenye nia njema, kushuhudia kwa nguvu zaidi ulimwenguni kote, maisha mapya na matumaini yaliyo ndani ya Kristo Yesu.

## AGANO LA USHIRIKA WA KANISA ANGLIKANA

### DIBAJI

**SISI,** tukiwa Makanisa ya Ushirika wa Kanisa Anglikana, chini ya BWANA wetu YESU Kristo, tuna ahidiana kwa pamoja na kwa dhati katika makubaliano yanayofuata. Tukiwa watu wa Mungu, tuliounganishwa kutoka *"kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha"*(Ufunuo 7:9), tunafanya hivi ili kuitangaza kwa nguvu zaidi, katika mazingira yetu mbalimbali, neema ya Mungu iliyofunuliwa katika Injili, kueneza upendo wa Mungu tunapohudumia mahitaji ya ulimwengu, kudumisha Umoja wa Roho Mtakatifu katika kifungo cha amani, na tukiungana na watu wote wa Mungu tuufikie ukamilifu katika Kristo. (Ef.4:3,13).

### SEHEMU YA KWANZA: Urithi wetu wa Imani

### 1.1. Kila Kanisa Linathibitisha:

1.1.1. Ushirika wake katika Kanisa Moja, Takatifu, Katholiko na Apostoliko, likiabudu Mungu mmoja wa kweli, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

1.1.2. Imani yake Katholiko na Apostoliko iliyofunuliwa kipekee katika Maandiko Matakatifu na kufafanuliwa katika Imani zinazotambuliwa na watu wote, Imani ambayo Kanisa linaitwa kuitangaza kwa upya kwa kila kizazi.[2] Mafundisho ya Kanisa la Uingereza[3], yaliyotungwa katika mazingira ya Matengenezo ya Kanisa ya Ulaya na yanayokubaliwa na kutumiwa kwa njia mbalimbali katika Ushirika Anglikana, yote hayo yanatoa ushuhuda wa kuaminika kwa imani hii.

1.1.3. Maandiko Matakatifu ya Agano la Kale na Agano Jipya kuwa yana mafundisho yote ya lazima kwa wokovu na kwamba ni kipimo cha mwisho cha imani[4].

1.1.4. Imani ya Mitume ikiwa ni alama ya Ubatizo; na Imani ya Nikea ikiwa ni Tamko linalotosheleza la Imani ya Kikristo.[5]

1.1.5. Sakramenti mbili zilizoamriwa na Kristo mwenyewe-Ubatizo na Chakula cha Bwana – zikihudumiwa bila kuacha kutumia maneno ya Kristo mwenyewe alipozindua Sakramenti hizi na viumbe alivyoviamuru Kristo[6].

1.1.6. Uaskofu wa Kihistoria, uliotengenezewa mfumo wa utumikaji wake unaozingatia mazingira na mahitaji mbalimbali ya mataifa na watu walioitwa na Mungu katika Umoja wa Kanisa lake.[7]

1.1.7. Taratibu zinazofanana za Sala kwa Watu Wote na Liturgia vinavyotajirisha na kudumisha Ibada yetu kwa Mungu na imani yetu na maisha yetu ya pamoja.

1.1.8. Kushiriki kwake katika Utume wa Mitume wa watu wote wa Mungu, na kwamba Utume huu ni wa kushirikiana na mapokeo mengine yaliyo nje ya Agano letu hili.

**1.2 Katika kuuishi Urithi wetu huu wa imani ya pamoja katika mazingira mbalimbali, kila Kanisa, kwa kumtegemea Roho Mtakatifu, Linajitoa kufanya yafuatayo:**

1.2.1. Kufundisha na kuenenda kwa namna ambayo inadumisha na inapatana na Maandiko Matakatifu na Imani Katholiko na Apostoliko, Huduma na Mapokeo kama yalivyo pokelewa na Makanisa ya Ushirika Anglikana, kwa kuzingatia Mabaraza ya pamoja ya Ushirika Anglikana na makubaliano yetu na Madhehebu mbalimbali.

1.2.2. Kuidumisha na kuieneza elimu ya theologia ya Kikristo na ya maadili na nidhamu inayotokana na inayopatana na Mafundisho ya Maandiko Matakatifu na Mapokeo ya Kanisa lote.

1.2.3. Kwa njia ya elimu hii kuona jinsi wanadamu na Ulimwengu wote ulioumbwa kwa njia ya kifo na ufufuo wa Kristo unavyofanywa upya, na kwa elimu hii pia kudhihirisha Utakatifu unaotolewa na Mungu na unaotazamiwa uonyeshwe na watu wake.

1.2.4. Kuyasikiliza vema, kuyasoma, kuyashika, kujifunza, na kuyahifadhi mioyoni mwetu Maandiko Matakatifu katika mazingira yetu mbalimbali, tukisaidiwa na usomaji wa makini na wa pamoja na juhudi ya mfano katika kuyasoma Maandiko Matakatifu, na kwa msaada wa mafundisho ya Maaskofu na Mabaraza ya Sinodi na matokeo ya uchambuzi mahili unaofanywa na wataalam walei au Wahudumu wasomi.

1.2.4. Kuhakikisha kwamba vifungu vya biblia vinapokelewa, vinasomwa, na vinatafsiriwa kwa uaminifu, uadilifu, ukamilifu na kwa upana wake tukitazamia kwamba maandiko yanaendelea kuliangaza na kulifanya upya Kanisa na watu wake, tamaduni na jamii kwa kupitia Maandiko hayo.

1.2.6. Kuhimiza na kuwa wazi kuhusu wito wa unabii na uaminifu wa Uongozi katika huduma na katika Utume ili kuwezesha watu wa Mungu kupokea kwa ujasiri nguvu ya Injili katika ulimwengu.

1.2.7. Kujitahidi kwa njia zote kudumisha wajibu wa kulea na kukuza Ushirika unaojali huduma ya Sakramenti kulingana na kanuni za nidhamu zilizopo kadri tunavyojitahidi, kwa msaada wa Mungu, kuufikia Ushirika wa Wakristo wote.

1.2.7. Kujitahidi kwenda pamoja na Mwili wote wa Kristo huku tukiendelea kutambua ukweli kamili unaofunuliwa na Roho Mtakatifu kwamba watu wa kutoka mataifa yote waweze kuwekwa huru na kupokea maisha mapya na tele katika Bwana wetu Yesu Kristo.

## SEHEMU YA PILI
### Maisha ya Ushirikiano na Wengine: Wito wetu wa Kianglikana

**2.1. Kila Kanisa linathibitisha:**

2.1.1 Ushirika ni kipawa cha Mungu kinachotolewa ili watu wa Mungu kutoka Mashariki na Magharibi, Kasikazini na Kusini, kwa pamoja, wautangaze utukufu wa Bwana na kuwa ishara ya ufalme wa Mungu katika Roho Mtakatifu na malimbuko ya kwanza katika ulimwengu ya kazi ya ukombozi wa Mungu ndani ya Kristo.

2.1.2 Shukrani zake kwa neema ya Mungu iliyotolewa kwetu nyakati zote; chimbuko letu katika Kanisa la Mitume; Mapokeo yetu ya zamani; historia ndefu ya Kanisa la Uingereza na Ireland iliyotajirishwa na Matengenezo ya Kanisa, na kukua kwetu kuwa Ushirika wa kimataifa kutokana na kazi ya ya mishoni ya upanuzi ya Kanisa; kuendelea kubadilishwa na Roho Mtakatifu kupitia vipawa na ushuhuda wa kujitoa mhanga wa Waanglikana ulimwenguni kote; na wito wetu wa kutaka kuyafikia maisha makamilifu ya Ushirika.

2.1.3 Kwa unyenyekevu wito wetu wa maisha ya toba wakati wote; kwa kushindwa kwetu kuonyesha uvumilivu na ukarimu na kumuona Kristo ndani ya wenzetu; matumizi yetu mabaya ya vipawa vya Mungu vilivyotolewa kwa neema; kushindwa kwetu kuitika wito wa Mungu wa kutumika; na tabia ya kila mtu kumnyonya mwenzake.

2.1.4 Umuhimu wa Utume wa Mungu ambao Ushirika wa Kanisa Anglikana unaitwa kuutekeleza, wito na baraka ya Utume unaowezesha kila Kanisa kuunganishwa na wengine katika Kristo kwa kazi ya kuueneza Ufalme wa Mungu. Kadri Ushirika wa Kanisa Anglikana unavyoendelea kupanuka na kuwa familia ya kimataifa yenye Makanisa yanayojitegemea, tunapokea changamoto na fursa za Utume mahali tulipo, katika nchi zetu na katika ngazi ya Kimataifa. Katika hili tunathamini urithi wetu wa Utume kuwa unawapa Waanglikana fursa dhahiri za ushirikiano katika Utume.

2.1.5 Kwamba Utume wetu wa pamoja ni Utume tunaoshirikiana na Makanisa mengine na Mapokeo mengine nje ya Agano hili. Tunapokea fursa za kutambua maisha ya Injili kamili, na ya upatanisho na ushirikiano na Kanisa la ulimwenguni kote kutekeleza katika Utume. Tunathibitisha wito wetu wa Waanglikana wa kuchuchumilia umoja unaoonekana wa Kanisa kama Kristo alivyosali kwamba **"Wote wawe na Umoja"**. Ni kwa kuwa na Watakatifu Wote kila mahali na muda wote ndipo tunapoweza kuutambua kwa kina zaidi ukombozi wa Kristo na upendo wake usio pimika.

**2.2 Kwa kutambua uthibitisho huu, kila Kanisa, kwa kumtegemea Roho Mtakatifu, linajituma:**

2.2.1 Kuitika wito wa Mungu, kufanya Uinjilisti na kushiriki katika kazi ya uponyaji na upatanisho "kwa ulimwengu wetu uliobarikiwa ingawa umepondeka, unaoumia na ulioanguka"[8], kwa njia ya uwajibikaji wa pamoja kushirikiana vipawa vya kiroho na vya mali vilivyotolewa na Mungu katika kazi hii.

**2.2.2** Kutekeleza Utume huu, "ambao ni Utume wa Mungu katika Kristo.[9]"

2.2.2. (a) "Kutangaza Habari Njema za Ufalme wa Mungu" na kuwaleta wote kwenye maisha ya Toba na Imani;

2.2.2. (b)"Kufundisha, Kubatiza na Kuwachunga Waumini," kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi (Math 28:19), kwa nguvu za Roho Mtakatifu,[10] na kuwaleta wote katika Mwili mmoja wa Kristo, wenye imani moja, wito mmoja, tumaini moja katika Bwana. (Ef.4:4-6).

2.2.2. (c) "Kuwahudumia watu katika mahitaji yao kwa matendo ya upendo". Kudhihirisha ufalme wa Mungu kwa huduma ya unyenyekevu kwa wote wenye uhitaji zaidi (Mrk 10:42-45; Math 18:4'25:21-45).

2.2.2. (d) "Kujitahidi kuleta mageuzi ya mifumo isiyowezesha haki kutolewa katika jamii, " kwa njia ya Kanisa, kusimama imara pamoja na Kristo kutangaza hukumu na wokovu kwa mataifa ya ulimwengu[11], na kudhihirisha nguvu ya roho inayoleta mageuzi kupitia matendo yetu tunayoyafanya kwa niaba ya haki ya Mungu.[12]

2.2.2. (e) "Kujitahidi kulinda ubora wa mazingira na kudumisha na kuendeleza uhai wa ardhi" zikiwa ni alama za lazima za utume wetu katika Ushirika wa Kanisa Anglikana.[13]

2.2.3 Kuutekeleza Utume huu kwa unyenyekevu na sisi wenyewe kuwa tayari, kwa pamoja, kuendelea kufanywa upya, tukizingatia ukengeufu na kushindwa kwetu katika kuwa mashahidi wa Injili.

2.2.4 Kuimarisha na kuunda upya mifumo yetu ya Utume itakayoweza kuwahamasisha na kuwapa changamoto watu wote wa Mungu waweze kufanya kazi, wasali, na watoe mali zao kwa kazi ya kuitangaza Injili.

2.2.5 Kuuimarisha Utume kwa njia ya Ibada yenye sifa na kicho kwa Mungu, tukimshukuru Mungu kwamba katika Sacramenti ya Ushirika wetu "Kristo ni chanzo na ndiyo lengo la umoja wa Kanisa na la kufanywa upya jamii ya wanadamu".[14]

## SEHEMU YA TATU: Umoja wetu na Maisha ya Ushirika

**3.1 Kila Kanisa Linathibitisha;**

3.1.1 Kwa kushiriki kwetu katika Ubatizo na Chakula cha Bwana, tunaingizwa katika Mwili mmoja wa Kanisa la Yesu Kristo, na tunaitwa na Kristo kufuata mambo yote yanayoleta amani na kujenga maisha yetu ya pamoja.

3.1.2. Dhamira yake ya kuishi katika Ushirika wa Makanisa.

Kila Kanisa, pamoja na Maaskofu wake wanaoongoza kwa kutumia Sinodi zao, linajipanga na kuweka mambo yake na wajibu wa Utume wake mahali lilipo kwa kutumia mfumo wake wa utawala na sheria na kwa sababu hiyo linajulikana kuwa ni "Ushirika unaojitegemea na unao wajibika"[15]. Kwa kumtegemea Roho Mtakatifu anayetuita na kutuwezesha tuishi maisha ya pamoja katika Ibada ya pamoja na ya kuombeana, katika upendano, kujituma na kutumika, tunataka kuimarisha maisha yetu ya pamoja kwa kutumia Vyombo vinne vya Ushirika wetu vinavyowezesha Makanisa yetu kuungana na mapenzi ya Kristo. Makanisa ya Ushirika wa Kanisa Anglikana yanafunga-manishwa "sio na mamlaka kuu moja yenye uwezo wa utendaji, bali na moyo wa kuheshimiana unaoimarishwa na mashauriano ya pamoja ya Maaskofu wanapokutana"[16] na yanafungamanishwa pia na Vyombo vingine vya Ushirika.

3.1.3 Wajibu wa msingi wa Maaskofu ni kuwa walinzi na wafundishaji wa imani, kuwa viongozi katika Utume, na kuwa alama ya wazi ya umoja, wakiliwakilisha Kanisa la ulimwenguni kote wanapokuwa katika Kanisa la mahali walipo, na pia wanaliwakilisha Kanisa la mahali walipo katika Kanisa la ulimwenguni pote, na kuwa kiungo cha Kanisa moja na Kanisa lingine mahali walipo. Huduma hii inatendeka kwa njia ya Askofu mwenyewe, Askofu akiwa pamoja na wahudumu wenzake, na Askofu akiwa ndani ya jamii ya Ushirika wa Waaminio, ambayo anaiwakilisha. Tunapokea na kudumisha huduma ya kihistoria iliyo na sehemu tatu: Maaskofu, Makasisi, na Mashemasi, wanaoamriwa kwa ajili ya huduma ndani ya Kanisa la Mungu, wakiwahimiza wote waliobatizwa kushiriki katika Utume wa Kristo.

3.1.4 Umuhimu wa Vyombo vya Ushirika Anglikana katika kusaidia kutambua, kufafanua na kuiishi Imani yetu ya pamoja na maisha ya Ushirika na Utume. Maisha ya Ushirika ni pamoja na kuwa tayari kutumia njia mbalimbali kutimiza mamlaka ya kimitume, kuanzia Mikutano ya Sinodi na Mikutano ya Maaskofu hadi kufikia kwenye huduma ya Kanisa moja moja kwa njia inayowezesha kufafanua na kuelezea imani ya washiriki wa Kanisa hilo kwa uamuzi wa pamoja(consensus fidelium). Pamoja na mahusiano ya aina mbalimbali yanayodumisha ushirikiano wetu, tunatambua Vyombo vinne maalum vinavyowezesha ushirikiano wetu katika maisha ya pamoja kwenye ngazi ya Ushirika wa Kanisa Anglikana.

I. Tunamtambua Askofu Mkuu wa Canterbury, kuwa Uaskofu Mkuu wa heshima na utii miongoni mwa Maaskofu wenzake wa Ushirika wa Kanisa Anglikana kwa kuwa wa kwanza kati ya walio sawa (Primus Inter Pares). Akiwa kiungo cha umoja, Askofu Mkuu huyu huitisha na kufanya kazi pamoja na Mikutano ya Maaskofu na Maaskofu Wakuu wote wa Ushirika wa Kanisa Anglikana na huwa Rais wa Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana (ACC).

II. Mkutano wa Lambeth wa Maaskofu wote huonyesha sura ya ushirikiano wa huduma ya Maaskofu ulimwenguni na huwakutanisha Maaskofu waabudu pamoja, washauriane, washirikishane na watiane moyo katika huduma yao ya kulinda imani na umoja wa Ushirika wa Kanisa Anglikana na kuwakamilisha Watakatifu ili kazi ya huduma itendeke. (Ef.4:12) na pia Utume ufanyike.

III. Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana lina Wajumbe Walei, Makasisi, na Maaskofu wanaowakilisha Makanisa yetu.[17] Linawezesha kazi ya pamoja ya Makanisa ya Ushirika wa Kanisa Anglikana, linaunganisha huduma ya kimataifa na madhehebu mengine na ya Utume wa Kanisa inayofanywa na Ushirika wa Kanisa Anglikana, linahimiza Makanisa kila moja kuwajibika kwa mwenzake na kutegemezana, na hutoa ushauri kuhusu maendeleo ya miundo ya Majimbo.[18]

IV. Mkutano wa Maaskofu Wakuu wa Majimbo huitishwa na Askofu Mkuu wa Canterbury kwa madhumuni ya kutiana moyo, kuomba pamoja na kushauriana. Mamlaka ya Maaskofu Wakuu wa Majimbo wanaoshiriki katika mikutano hii inatokana na nafasi zao kuwa ndio Maaskofu Viongozi wa Majimbo yao na kwamba wana ushirikiano na mikutano yao ya Maaskofu katika Jimbo kwa kufuata miundo ya Sinodi zao.[19] Wakati wa Mkutano wao, Maaskofu Wakuu wa Majimbo na Wakuu wengine wa Makanisa wanaoitwa "Moderators" wanatazamiwa kufanya kazi kama wawakilishi wa Majimbo yao kwa kushirikiana kila mmoja na mwenzake katika Utume na katika mambo ya imani, mambo ya maadili na mambo ya kichungaji yanayogusa Ushirika wa Kanisa Anglikana wote.

Ni wajibu wa kila Chombo kushauriana, kupokea maoni, na kusaidiana na Vyombo vingine na Makanisa ya Ushirika wa Kanisa Anglikana.[20] Kila Chombo kinaweza kikaanzisha na kupendekeza mchakato wa kupata maoni na mwelekeo wa Ushirika wa Kanisa Anglikana na Makanisa yake.

**3.2. Tukitambua maisha yetu ya kutegemeana, kila Kanisa, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, Linajituma:**

3.2.1 Kuzingatia faida ya Ushirika wa Kanisa Anglikana wote linapofuata haki yake ya kujitegemea, kusaidia kazi ya Vyombo vya Ushirika wa Kanisa Anglikana kwa hali na mali kadri ya uwezo wake, na kupokea kazi ya Vyombo hivyo likiwa tayari kutafakari maamuzi ya Vyombo hivyo na kuona jinsi ya kuyatumia mapendekezo ya Vyombo hivyo katika huduma yake.

3.2.2 Kuheshimu mamlaka ya mwisho Kikatiba ya Makanisa yote ya Ushirika wa Kanisa Anglikana, huku tukizingatia uwajibikaji wetu wa pamoja na kutegemeana katika Mwili wa Kristo,[21] na wajibu wa kila mmoja kwa Ushirika wa Kanisa Anglikana kwa jumla.[22]

3.2.3 Kutumia muda wakati wa majadiliano na tafakari za kitheologia kujiweka tayari kusikiliza na kuwa mvumilivu, kuomba na kujifunza pamoja na wengine ili kutambua mapenzi ya Mungu. Aina hiyo ya maombi, kujifunza na kujadiliana ni sura muhimu ya maisha ya Kanisa linapotafuta kuongozwa na Roho Mtakatifu katika kweli yote na kutangaza Injili kwa upya kwa kila kizazi. Masuala mengine, yanayoonekana ni ya mgongano au mapya yanapojitokeza, yanaweza yakasababisha uelewo wa kina kabisa wa maana ya mafunuo ya Mungu kwetu; mengine yanaweza kujitokeza kuwa ni mapotofu na hata yakawa mapingamizi kwa imani. Kwa hiyo, mambo yote hayo yanahitaji kupimwa kwa uelewa wa pamoja katika maisha ya Kanisa.

3.2.4 Kutafuta utambuzi wa pamoja na makanisa mengine, kupitia Mabaraza ya Ushirika wa Kanisa Anglikana, kuhusu mambo yanayotuhusu sote, kwa njia ambayo inapatana na Maandiko Matakatifu, Vigezo vya kawaida ya imani, na kanuni na sheria za Makanisa yetu. Kila Kanisa litajitahidi kushauriana na Makanisa mengine ya Ushirika wa Kanisa Anglikana na Vyombo vya umoja na Tume za Ushirika wa Kanisa Anglikana.

3.2.5 Kuenenda kwa uadilifu, uangalifu, na tahadhari kuhusu tendo lolote lile ambalo lingeweza kuzusha mgogoro, ambao kwa kutegemea na ukubwa wake, kiini chake na upana wake, mgogoro huo unaweza kutishia Umoja wa Ushirika wa Kanisa Anglikana na ufanisi au heshima ya Utume wake.

3.2.6 Kunapotokea migongano kuwa tayari kushiriki katika mazungumzo ya ufumbuzi wake, ambayo inaweza kuhusu mikutano ya ana kwa ana, kukubaliana vigezo na utayari wa kuona kwamba mchakato huo unafikishwa mwisho.

3.2.7 Kuzingatia kwamba vifungo vyetu vya upendo na upendo wa Kristo vinatubidiisha siku zote kufikia kiwango cha juu sana iwezekanavyo cha Ushirika.

**SEHEMU YA NNE: Maisha yetu ya Pamoja chini ya Agano**

**4. Kila Kanisa linathibitisha Misingi na Taratibu, na, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, Linajituma kuyatekeleza yafuatayo:**

**4.1 Kuridhia Agano**

4.1.1 Kila Kanisa linaloridhia Agano hili linathibitisha kuwa linaingia katika Agano ikiwa ni kuingia katika uhusiano chini ya mamlaka ya Mungu. Kila Kanisa linatoa uthibitisho huu kwa Makanisa mengine ili liishi maisha ya utimilifu zaidi katika Ushirikiano wa Makanisa na kutegemeana, ambao ni msingi wa Makanisa ya Ushirika wa Kanisa Anglikana. Ushirika wa Kanisa Anglikana ni mshikamano ndani ya Kanisa moja, Takatifu na Apostoliko, lenye Makanisa yaliyo ndani ya taifa moja au mataifa mengi, ambayo kila moja linatambua ndani ya wenzake vifungo vya umoja vya utii kwa Kristo vinavyoonyeshwa katika Imani na huduma na urithi mmoja wa ibada, maisha na utume, na utayari wa kuishi katika hali ya kutegemeana.

4.1.2 Kwa kuridhia Agano hili, kila Kanisa linathibitisha kuwa linayakubali yaliyosemwa katika Sehemu tatu zilizo-tangulia, za Imani, Utume na Kutegemeana, na kwamba yaliyosemwa yanapatana na maisha yake lenyewe na imani na vitendo vya imani ya Kikristo kama ambavyo Kanisa hilo limevipokea, na linatambua Sehemu zote hizo kuwa ni za msingi kwa maisha ya Ushirika wa Kanisa Anglikana na kwa maisha ya ushirikiano kati ya Makanisa yanayolikubali Agano hili.

4.1.3 Kutambuana na kuheshimiana huko, hakuna maana ya Kanisa moja kujiweka chini ya mamlaka yoyote ya nje ya mipaka yake. Hakuna chochote katika Agano hili kitakachosomeka kuwa kinabadilisha Katiba na Kanuni za Kanisa lolote lile la Ushirika wa Kanisa Anglikana, au kupunguza uhuru wa utawala wake. Agano hili halitoi kwa Kanisa lolote lile au Chombo chochote kile cha Ushirika wa Kanisa Anglikana, utawala au usimamizi wa Kanisa lolote lile la Ushirika wa Kanisa Anglikana.

4.1.4 Kila Kanisa lililo katika Ushirika wa Kanisa Anglikana, kama linavyotambuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana (ACC), linakaribishwa kuingia katika Agano hili kwa kufuata Katiba na Taratibu zake.

4.1.5 Vyombo vya Ushirika wa Kanisa Anglikana vinaweza kuyakaribisha Makanisa mengine kuingia katika Agano hili kwa kutumia taratibu zile zile zilizowekwa na Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana kunapokuwa na marekebisho ya orodha ya wanachama wake. Kuingia katika Agano hili hakutoi haki ya kutambuliwa au haki ya uanachama wa Vyombo vya Ushirika wa Kanisa Anglikana. Kutambuliwa au kuwa Mwanachama wa Vyombo hivyo kutaamuliwa na Vyombo vyenyewe.

4.1.6 Agano hili linaanza kufanya kazi pale ambapo Kanisa linaliridhia kwa kufuata Katiba, Kanuni na Taratibu zake.

**4.2. Udumishaji wa Agano na Utatuzi wa Migogoro**

4.2.1 Agano linafanya kazi ya kuonyesha makubaliano ya pamoja na uwajibikaji wa pamoja unaolifanya kila Kanisa liwe katika uhusiano wa Ushirika na Makanisa menzake mengine. Kulitambua na kuliheshimu Agano hili kunawezesha kutambuana na kushirikiana kwa Makanisa husika. Kuingia katika Agano hili kuna maana ya kila Kanisa kutambua vitu ambavyo lazima vidumishwe katika maisha yake na ambavyo Kanisa hilo litawajibika kwavyo kwa Makanisa ambayo yamo katika Ushirika wa Kanisa Anglikana ili kudumisha uhusiano unaoonyeshwa katika Agano hili.

4.2.2 Kamati ya Kudumu ya Ushirika wa Kanisa Anglikana, inayowajibika kwa Baraza la Mashauriano na kwa Mkutano wa Maaskofu Wakuu, itafuatilia jinsi Agano hili linavyofanya kazi katika maisha ya Ushirika wa Kanisa Anglikana kwa niaba ya Vyombo vya ushirikiano. Katika wajibu huu Kamati ya Kudumu itasaidiwa na Kamati au Tume nyingine kadri itakavyoamriwa katika utekelezaji wa wajibu wa kazi hii na kuishauri hiyo Kamati kuhusu maswala yanayohusu Agano hili.

4.2.3 Maswali yakiibuka yanayohusu maana ya Agano hili, au tendo la Kanisa moja lililoingia katika Agano linavyopatana na Agano lenyewe, itakuwa ni wajibu wa kila Kanisa linaloingia katika Agano kujitahidi kuheshimu uthibitisho wake uliotolewa katika Sehemu ya 3.2. Maswali yanayoibuka yanaweza kuletwa na Kanisa lenyewe, au Kanisa lingine lililo katika Agano, au na Vyombo vya Ushirika wa Kanisa Anglikana.

4.2.4 Ikiwa hakuna makubaliano basi jambo hilo litapelekwa kwa Kamati ya Kudumu. Kamati ya Kudumu itafanya kila jitihada kuwezesha makubaliano, na inaweza ikatafuta ushauri kwa Vyombo vingine kadri itakavyoona inafaa katika kufikia uamuzi wa kuliona jinsi shauri lenyewe lilivyo na matokeo yake katika mahusiano. Kadri itakavyoonekana inafaa, Kamati ya Kudumu italipeleka jambo hilo kwa Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana na kwa Mkutano wa Maaskofu Wakuu, kwa Ushauri.

4.2.5 Kamati ya Kudumu inaweza kuliomba Kanisa husika kuahirisha utekelezaji wa tendo linaloleta mgongano. Ikiwa Kanisa hilo litakataa kuahirisha utekelezaji wa tendo lake, Kamati ya Kudumu itapendekeza kwa Vyombo vya Ushirika, ikionyesha matokeo ya hatua hiyo katika mahusiano. Kamati inaweza kupendekeza kushiriki kwa sehemu tu au kusimamishwa kwa Kanisa hilo katika shughuli za Chombo kinachohusika mpaka mchakato unaoelezwa hapa chini utakapokamilika.

4.2.6 Kwa kufuata msingi wa ushauri uliotolewa na Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana na Mkutano wa Maaskofu Wakuu, Kamati ya Kudumu inaweza kutamka kuwa tendo au uamuzi husika hauendani na Agano.

4.2.7 Kutokana na ushauri uliopokelewa, Kamati ya Kudumu itatoa mapendekezo yanayobainisha matokeo ya mahusiano yatakavyo athiriwa na kitendo ambacho hakipatani na Agano. Mapendekezo haya yanaweza kupelekwa kwa Makanisa Wanachama wa Ushirika wa Kanisa Anglikana au kwa Vyombo vya Ushirika wa Kanisa Anglikana na kuelezea kiasi gani uamuzi wa Kanisa lolote unavyoweza kuathiri au kupunguza ushirika kati ya Kanisa hilo na Makanisa mengine ya Ushirika wa Kanisa Anglikana, na matokeo mengine. Kila Kanisa au kila Chombo kitaamua kama kiyakubali au kisiyakubali mapendekezo hayo.

4.2.8 Watakaoshiriki katika maamuzi ya Kamati ya Kudumu au ya Vyombo vya Ushirika kuhusiana na Sehemu ya 4.2, watakuwa ni wajumbe wale tu wa Vyombo vya Ushirika wanaowakilisha Makanisa yaliyoingia katika Agano au Makanisa yanayoendelea na mchakato wa kuingia katika Agano.

4.2.9 Kila Kanisa linakubali kuweka utaratibu, vyombo au asasi, kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zake, kwa wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa Mambo ambayo Kanisa lilithibitisha na yale ambayo lilijituma kufanya; na vyombo au asasi hizo zitadumisha mawasiliano na Vyombo vya Ushirika Anglikana kwa masuala yanayohusu Agano.

**4.3. Kujiondoa katika Agano**

4.3.1 Kanisa lolote linaloingia katika Agano hili linaweza kuamua kujiondoa katika Agano. Japo kama kujitoa huko hakutakuwa na maana ya kujitoa moja kwa moja kutoka Vyombo vya Ushirika wa Kanisa Anglikana, au kuwa na maana ya kuukana Uanglikana wake, hata hivyo kujitoa huko kunaweza kukazua swali kuhusu maana ya Agano, na kuhusu kama vinapatana na misingi ya Agano iliyowekwa humu, na kusababisha utekelezaji wa vifungu vilivyo katika sehemu ya 4.2 hapo juu.

**4.4. Andiko la Agano na namna ya Kulirekebisha**

4.4.1 Agano lenyewe hasa linaanzia na Dibaji, kisha zinafuata Sehemu 4, na hatimaye Tamko. Utangulizi wa Agano, ambao wakati wote utakuwa ukiambatanishwa na Agano, sio sehemu rasmi ya Agano. Mamlaka na umuhimu wake vitatokana na kule kusaidia kuelewa madhumuni ya Agano.

4.4.2 Ye yote kati ya Kanisa linaloingia katika Agano hili au Chombo chochote cha Ushirika anaweza kupeleka pendekezo la kurekebisha Agano kwa Vyombo vya Ushirika kupitia Kamati ya Kudumu. Kamati ya Kudumu italipeleka pendekezo hilo kwenye Baraza la Mashauriano la Kanisa Anglikana, kwenye Mkutano wa Maaskofu Wakuu, kwa Makanisa yaliyoingia katika Agano na kwa Chombo chochote kile kadri itakavyoona inafaa kwa ajili ya kupata ushauri. Kamati ya Kudumu itatoa maoni yake kuhusu pendekezo lililotolewa kwa mujibu wa ushauri uliopatikana, na kulifikisha pendekezo hilo na marekebisho yoyote yaliyofanyika kwa Makanisa yaliyoingia katika Agano. Badiliko litafanya kazi litakapo thibitishwa na robo tatu ya Makanisa yaliyo katika Ushirika wa Kanisa Anglikana. Kamati ya Kudumu itaweka utaratibu wa namna ya kulitangaza badiliko lililopitishwa.

**TAMKO LETU**

KWA FURAHA NA KWA NIA THABITI TUNATAMKA KUWA MAKANISA YETU NI WASHIRIKI WA AGANO HILI LA USHIRIKA ANGLIKANA, TUKIWA TAYARI SISI WENYEWE KWA UTUMISHI UZAAO MATUNDA NA KUSHIKAMANA WENYEWE KARIBU ZAIDI KATIKA UKWELI NA UPENDO WA KRISTO. UTUKUFU UWE KWA BABA NA MWANA NA ROHO MTAKATIFU, MILELE NA MILELE. AMIN.

*"Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi*

*yake; naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; Utukufu una Yeye milele na milele. Amin."* (Hebr. 13:20,21).

## Kumbukumbu za Rejea

[1] *The Church of the Triune God*, The Cyprus Statement of the International Commission for Anglican Orthodox Theological Dialogue, 2007, paragraph 1,2.

[2] Cf. The Preface to the Declaration of Assent, Canon C15 of the Church of England.

[3] The Thirty-nine Articles of Religion, the 1662 Book of Common Prayer, and the Ordering of Bishops, Priests, and Deacons

[4] The Chicago-Lambeth Quadrilateral of 1886/1888
[5] The Chicago-Lambeth Quadrilateral of 1886/1888

[6] cf. The Chicago-Lambeth Quadrilateral 1886/1888, The Preface to the Declaration of Assent, Canon C15 of the Church of England.

[7] cf. The Chicago-Lambeth Quadrilateral 1886/1888

[8] IASCOME Report, ACC-13

[9] The five Marks of Mission are set out in the MISSIO Report of 1999, building on work at ACC-6 and ACC-8.

[10] *Church as Communion* n26

[11] WCC 1954 Evanston, *Christ the Hope of the World*
[12] Moscow Statement, 43

[13] IARCCUM, *Growing Together in Unity and Mission*,118

[14] Baptism, Eucharist and Ministry, WCC,

[15] A Letter from Alexandria, the Primates, March 2009

[16] Lambeth Conference 1930

[17] Constitution of the ACC, Article 3 and Schedule
[18] cf. the Objects of the ACC are set out in Article 2 of its Constitution.

[19] Report of the Windsor Continuation Group, 69.

[20] cf IATDC, Communion, Conflict and Hope, paragraph 113.
[21] Toronto Congress 1963, and the Ten Principles of Partnership.

[22] cf. the Schedule to the Dar es Salaam Communiqué of the Primates' Meeting, February 2007